


PIMA VWU, UJUE AFYA YAKO



**UPIMAJI NA USHAURI NASAHA WA VWU
KWA WANAUME WANAJOJAMIANA NA
WANAUME WENZAO**



Tume ya UKIMWI Zanzibar



Simu: +255 24 223 5694, Barua pepe: info@zac.or.tz

[f](#) TumeyaUkimwi Zanzibar [i](#) Zanzibar_aids_commission [v](#) TumeyaUkimwi Zanzibar [g](#) www.zac.or.tz

UTANGULIZI

Hapa Zanzibar, tafti zinaonyesha kwamba maambukizo ya Virusi Vinavyosababisha UKIMWI (VVU) miongoni mwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao ni makubwa. Katika kila watu 100, wanaofanya mapenzi ya aina hii watu 5 wameambukizwa VVU. Kundi hili limeathirika sana na maambukizo ya homa ya ini B na C (hepatitis B na C) pamoja na magonjwa ya kujamiiana.

Wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao wako kwenye hatari ya kuambukiza ama kuambukizwa VVU na magonjwa mengine ya kujamiana. Hatari yao ipo katika tabia hatarishi walizo nazo. Hata hivyo, kutokana na mazingira yaliopo hawapati ipasavyo huduma ya kupima VVU na kujua hali za afya zao.

SABABU ZINAZOWAWEKA KATIKA HATARI YA KUPATA VVU

- Kujamiiiana kinyume na maumbile. Kitendo hichi kinapelekea kupata michubuko kwa urahisi ambayo hurahisisha maambukizo ya VVU.
- Kuwa na uhusiano wa wapenzi wengi kwa wakati mmoja (Mchati)
- Kutotumia kondomu.
- Kufanya ngono za makundi (Mtungo)
- Utumiaji wa vileo.
- Kutotibu na maradhi ya kujamiiana

MAANA YA UPIMAJI NA USHAURI NASAHA

Ni huduma ya hiari na ya usiri inayotolewa kwa mtu mmoja mmoja au wenza wanaotaka kujua hali zao za afya kama wameambukizwa VVU au hawajaambukizwa.

MAANA YA UPIMAJI NA USHAURI NASAHA

- Nitapata ushauri utaoonisaidia kuondosha hofu na wasi wasi ikiwa nimeambukizwa au la
- Nitapata kujua hali yangu ya maambukizo ya VVU.

KUMBUKA:

AFYA YAKO NI MTAJI WAKO "PIMA VVU UJEE AFYA YAKO!"

- Nitaacha tabia hatarishi na kujikinga na maambukizo mapya ya VVU.
- Nitaanza kutumia dawa za ARV mapema iwapo nitagundulika na maambukizo.
- Nitapata huduma nyengine za magonjwa nyemelezi kama vile Kifua Kikuu, Homa ya Ini, magonjwa ya kujamiiana nk.
- Itanisaidia kupata huduma za kijamii zinazohusu VVU na UKIMWI.

HASARA GANI NITAZIPATA NISIPOPIMA VVU MAPEMA?

- Ninaweza kuambukiza au kuambukizwa VVU.
- Nitakosa haki za msingi za huduma ya kinga na tiba ya VVU na magonjwa ya kujamiiana.
- Ninaweza kupata magonjwa nyemelezi.
- Nitakosa huduma kwa wakati na itapelekea afya yangu kudhoofika.
- Ninaweza kujiingiza katika tabia hatarishi za maambukizo ya VVU na UKIMWI.

NICHUKUE HATUA GANI?

- Niwe na tabia ya kupima VVU mara kwa mara.
- Niende kupima katika vituo vya Afya.
- Nijiepushe kufanya ngono zisizo salama.
- Nitumie huduma za kinga na tiba ya VVU zilizokaribu.
- Inanipasa nitumie kondom moja kwa usahihi kila tendo la kujamiiana.

NITAPATA WAPI HUDUMA RAFIKI ZA VVU NA UKIMWI?

- Vituo mbalimbali vya Afya vya Serikali na binafsi.
- Asasi za kiraia (zisizo za Serikali) kama vile ZAYEDES, ZANGOC, AYAHIZA, ZYF, ZAPHA+ kwa Unguja na ZAYEDES, ZAPHA+, na UMATI kwa Pemba.
- Huduma za Upimaji za masafa (Outreach) zinazotolewa na Asasi zisizo za kiserikali kwenye sehemu za starehe na mikusanyiko ya watu.